



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII  
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA**



**TANGAZO LA MNADA WA MITI YA MISAJI YENYE META ZA UJAZO 2,000.9 KATIKA  
KIUNGA NAMBA (MT11 - A1, A2, A3, A4 & A5) NA KIUNGA NAMBA (MT11 B2, B3 & B4)  
ZILIZOPO KATIKA SHAMBA LA MITI MTIBWA TURIANI - MOROGORO**

**MNADA NA.02 2016/17**

**Tarehe: 12/07/2016**

1. Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) unatarajia kuuza meta za ujazo 2,000.9 za miti aina ya misaji katika Shamba la Miti la Mtibwa siku Jumatatu tarehe 25/07/2016 kuanzia saa 4: 30 asubuhi.
2. Kampuni au mtu binafsi anaetaka kushiriki mnada atawasilisha nyaraka zake kwenye bahasha iliyofungwa ikiwa pamoja na kielelezo cha usajili wa biashara ya mazao ya Misitu kwa mwaka 2016/2017 na cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN ). Watakaochelewa hawatapokelewa.
3. Mnada utaendeshwa hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika ofisi ya Meneja wa shamba siku ya Jumatatu tarehe 25 Julai 2016 na utaendeshwa kwa kufuata sheria ya Misitu Sura ya 323.
4. Kila kiunga kitanadiwa peke yake kulingana na bei ya Ujazao iliyopo. Hata hivyo, bei ya juu iliyotolewa na mnunuzi wakati wa kufungua bahasha haitazuia wanunuzi wengine kuongeza bei zaidi ya iliyotajwa awali.
5. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania unawaalika wanunuzi kwenye mnada katika Shamba la miti Mtibwa ambapo mnunuzi anaweza kuchagua mojawapo kati ya viunga vifuatavyo;

### KIUNGA NAMBA MT11 A1-A5 NA MT11 B2-B4

NA.	JINA LA KIUNGA	NAMBA YA KITALU	META ZA UJAZO
1	MT 11	A1	200.0701
2	MT11	A2	200.0523
3	MT11	A3	200.0814
4	MT 11	A4	200.4866
5	MT 11	A5	200.0629
6	MT 11	B2	300.0339
7	MT11	B3	400.01
8	MT 11	B4	300.1139
<b>JUMLA KUU</b>			<b>2000.9111</b>

**Angalizo: Kila kiunga kitauzwa peke yake.**

6. Wakala wa Huduma za Misit Tanzania utatoa hati ya ushindi kwa mnunuzi aliyetaja kiwango cha juu kwa kila kiunga wakati wa mnada.
7. Mnunuzi atakayefanikiwa hataruhusiwa kusafiirisha magogo kwa mujibu wa kanuni namba 50(1) ya mwaka 2004. Kusafirisha Mazao ya Misitu itakuwa kwa mfumo wa malighafi mbao kwa Mujibu wa Tangazo la serikali Na 69 la mwaka 2006.
8. Watu binafsi na makampuni wanakaribishwa kutembelea viunga shambani wakati wa saa za kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:00) alasiri isipokuwa siku za sikukuu. Meneja wa shamba au msaidizi atakuwepo kwa ajili ya maelekezo zaidi.
9. Wanunuzi wanapaswa kuchukua na kusoma masharti ya uvunaji kwa kila shamba yatakayopatikana kwa Meneja wa shamba husika.
10. Bei ya kianzio kwa meta moja ya ujazo ni TZS 500,000/= (shilingi za kitanzania LAKI TANO tu) inayojumuisha ongezeko la thamani VAT, CESS NA LMDA.
11. Mnunuzi atakayeshinda atalipa asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani yote ya ununuzi siku tatu (3) baada ya mnada kufanyika. Fedha hizo hazitarudishwa. Asilimia sabini na tano

(75%) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya mnada. Malipo yatafanyika katika Akaunti ya shamba la Miti husika kama inavoonekana hapa chini;

**SHAMBA LA MITI MTIBWA,**

**AKAUNTI NA. 22010000567**

**NMB – TURIANI**

12. Mnunuzi atapaswa kuwasilisha hati ya malipo (pay – in – slip) ya benki kwa meneja wa shamba kama uthibitisho wa malipo si zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.
13. Wanunuzi watakaoshinda watasaini mkataba na Wakala wa Huduma za Misitua Tanzania siku kumi na nne (14) baada ya kulipa salio la asilimia sabini na tano (75%) ya gharama zote.
14. Tangazo la mnada huu linapatikana katika tovoti zifuatazo: [www.tfs.go.tz](http://www.tfs.go.tz), na [www.mnrt.go.tz](http://www.mnrt.go.tz)

Imetolewa na;

Kaimu Mtendaji Mkuu,

Wakala wa Huduma za Misitua Tanzania (TFS),

S.L.P 40832 dar Es Salaam.

Simu: +255 22 286 4249; Nukushi: +255 22 2864257; Barua pepe: [mpingo@tfs.go.tz](mailto:mpingo@tfs.go.tz)

Tovuti: [www.tfs.go.tz](http://www.tfs.go.tz)